

KITONGOJI CHA UVINJE
KIJIJI CHA SAADANI
WILAYA YA BAGAMOYO
MKOA WA PWANI
22/6/2004

MKUU WA WILAYA
WILAYA YA BAGAMOYO
MKOA WA PWANI

**YAH: FITINA YA FIDIA ZA MAMILIONI YA TANAPA MMOJA AFARIKI
KATIKA MALUMBANO.**

Mhe: Mkuu wa Wilaya.

Heshima nyingi juu yako naomba uhusike na somo la hapo juu.

Kwa masikitiko makubwa sisi wanakitongoji na wote wapenda amani na utulivu nchini, tunalaani juu ya kitendo cha Tanapa kuvamia Kitongoji chetu bila ridhaa ya wengi na kuthamini nyumba na mazao ya watu ambao hawaishi Kitongojini na wengine hawatambuliki kama wenye chochote cha kuza, hapa na wana makwao kwa baba zao.

Mmoja wa watetezi ndugu yetu Jumaa Shehe Babu Kiongozi wa CCM huko Tandika Dar es Salaam anakoishi kakashifiwa na mmoja wa mamluki wa Tanapa na akafa ghafla mbele ya watu wote wakiangalia tarehe 22/5/2004 Kitongojini Uvinje.

Kitendo hicho uchungu wake hautasahaulika daima. Ndugu. Jumaa hakuja hapo ili afe, wala hakua na taarifa yoyote iliohusu kuthamini mali siku hiyo. Yeye alifika kusalimia ndugu baada ya muda mrefu kutofika hapo. Hii ni kinyume na mawazo potofu yaliyojengwa na Tanapa na genge lake. Hao watu wa Uvinje feki hawamo katika orodha iliopo katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mkoa, Mbunge, Maliasili na Tanapa.

Fitina kubwa imezushwa na shirika hilo la Umma bila sababu za maana. Hadi sasa ndugu hawasalimiani kwa uchochezi huo wa pesa za umma. Tarehe 17/5/2004 meneja Mkuu alitangaza kumalizika kwa zoezi la kulipa fidia tliyogharimu shilingi Millioni mia mbili kwa Tanapa Saadani. Tanapa ikakusanya na kushawishi watu wanaohusika kidogo na wasiohusika kwa uvinje ili nao wachote mapesa hayo. Bila kujali nini kitatokea.

Fedha Fedheha. Watu walihamasika na kuanza kuingia maporini na Koko na kuharibu kwa kukata mikoko yote na miti ya hifadhi bila Tanapa kujali kwa dhamira ya Tanapa ni kukomoa wanaojidai kichwa ngumu ushahidi upo. Jeuri ya pesa wakaonyesha Tanapa na genge lao. Hata lile agizo la Mh. Kikwete tarehe 21/3/2003 ambalo Tanapa wanalo wakalidharau na matokeo yake kusababisha kifo cha ndugu yetu na kuleta uhasama mkubwa miongoni mwetu. Mh. Mkuu wa Wilaya tunasema walioandika barua za kuomba kuuzâ mali zao si watu wa uvinje.

Kwa sababu vikao vimefanyika Kitongojini hakuna alietaka kuuza chochote. Kikao cha kwanza cha Mkuu wa Wilaya Mama Mesaki, Pili Mkuu wa Mkoa Bw. Banduka Cha tatu Mama Mesaki na cha nne Mbunge Mh. Kikwete vyote kauli ya wanauvinje ni moja ya kutouza mali zao. Hawa walikua wapi kama si uchochezi. Hadi sasa hakuna kilichofuatiliwa waliosababisha kifo, ikizingatiwa mtu alikufa mbele ya Polisi.

Tunasisitiza hatuna ugomvi na yoyote, lakini unyonge wetu usitumiwe na yeyote kutunyanyasa, kututisha kwa mapesa na chochote. Hoja yetu ni kwa hifadhi toka ianze sisi tunatambuliwa kua tupo nje ya hifadhi. Ramani na alama za mipaka ni ushahidi tosha wanazo. Pili tunatekeleza agizo la Mbunge tuliomchagua kua msiuze maeneo yenu ya Pwani kwani ni alimasi kwenu na vizazi vyenu daima katika kampeni ya Ubunge mwaka 2000.

Tatu hatuna sababu ya kuhamishwa bila ya kosa lolote ili hali katika hao wanaotuona sisi ni duni kuliko ngedere hawakuleta Mnyama kazi ya kulinda wanyama hawa tuliifanya wenyewe bila ya Tanapa.



Nne tunatekeleza ahadi waliopewa wazazi wetu na muanzilishi wa hifadhi Bw. MAHINDA kua eneo hili lipo nje ya hifadhi kwa faida yetu na vizazi zijavyo na Taifa zima au yeletwe maandishi Mmbadala, ya kauli hii ya Mahinda kwa wazazi wetu.

Hii ina maana wananchi wakitongoji ndio walioiomba Serekali kutuhifadhia Wanyama wetu kwa uchungu wa kuwindwa ovyo na watu toka Pangani, Tanga na Mombasa.

Mwisho tunalaani vitendo vinavyofanywa na chombo hiki muhimu cha serekali yetu na kuchochea uhasama wa ndugu. Tunakuomba Mkuu wetu wa Wilaya ulione hilo na kulifanyia kazi na wote waliohusika bila kujali cheo, fedha na kadhalika aliesababisha kifo cha ndugu yetu achukuliwe hatua na kukomeshwa kwa fitina hizo mara moja bila kuwasahau walioharibu mazingira kwa kukata miti ya Mikoko na miti ya hifadhi ili kujenga nyumba harakaharaka kwa tamaa ya kuziua kwa Tanapa. Maana huenda fitina kama hii ikarudia tena itakuaje? Matumaini ya wananchi na ari ya awali yanapungua juu ya uongozi wa Tanapa.

Tuko tayari kuzungumza na yeyote kuhusu uendelezaji wa eneo letu hilo nje ya hifadhi kwa faida yetu, vizazi vyetu na Taifa bila ya kuathiri viumbe na mazingira yake.

Tunakutakia kazi njema.

Hussein Swalehe Akida.
Mwenyekiti wa Kitongoji.

Nakala:

Mhe: Mbunge Chalinze

Waziri wa Maliasili na Utalii.

Waziri wa Mambo ya ndani

Mkuu wa Mkoa wa Pwani

Tanapa Makao Makuu

Wahariri -Magazeti ya Nipashe, Mtanzania na Uhuru.

UVINJE SUB-VILLAGE

SAADANI VILLAGE

BAGAMOYO DISTRICT

COAST PROVINCE

22/6/2004

PROVINCIAL COMMISSIONER

BAGAMOYO DISTRICT

COAST PROVINCE

RE: RUMOURS ABOUT THE MILLIONS OF COMPENSATION FOR TANAPA WHERE ONE WAS LEFT DEAD IN THE FRACAS

Honourable: Provincial Commissioner.

With all due respect, I pray that you look into the above mentioned matter.

It is with deep regret that we, the villagers and all who love peace and tranquility in the country. We condemn the act at Tanapa of invading our sub-village without compensation for all for the houses and produce of people who do not stay in the village and others are not recognized as having anything to sell here yet they live at there fathers homesteads.

One of our own defenders brother Jumaa Shehe, elderly leader of CCM in Tandika Dar es Salaam where he stays, was accosted by one of the gang of Tanapa and he died suddenly before the very eyes of the villagers on 22/5/2004 in Uvinje sub-village.

The pain of that act will forever remain with us. Brother Jumaa did not go there to die; neither did he have any information as to the compensation on that day. He came to greet the brother after a long time. This is against the wrong impression created by Tanapa and its gang. The ghost Uvinje villagers do not exist in the list at the District Commissioner's office, province, member of parliament, or Tanapa's natural resources

A lot of lies have been peddled by that public organization without any concrete reason. Until now, people are not even greeting others because of the fury of the public funds. On 17/5/2004 the senior manager announced the conclusion of the exercise of compensation to the tune of two hundred million (200 million) for Tanapa Saadani. Tanapa gathered and convinced those less involved and even those not involved in Uvinje so that they can benefit from the money, without considering the implication.

Money brings problems. People got aware of that and went to the forest with axes and felled trees without Tanapa caring that their (Tanapa's) intention is to beat up those who think they are thick headed, there's evidence to that effect. Tanapa and its gang showed their pride in money. Tanapa even did not give heed to Honourable Kikwete's advice on 21/3/2003 which they are fully aware of and the resultant was causing the death of our brother and bringing a lot of anguish and enmity amongst us. Honourable District Commissioner, what we are saying is that those who wrote letters to ask that they be compensated are not indeed residents of Uvinje.

We have had meetings in the sub-village and nobody wants to sell anything. The first meeting with the District Commissioner Mama Mesaki, the second one with the Provincial Commissioner Mr. Banduka, the third one with Mama Mesaki and the fourth with member of parliament Honourable Kikwete. In all sittings, Uvinje villagers were unanimous that they won't sell their property. Where were they? Until now, nothing has been done about those who caused the death, notwithstanding that someone died before the very eyes of the police.

We insist that we do not have any problem with anybody, but our feebleness should not be used by anyone to frustrate us, using money or anything. Our major concern is that since the establishment of the Reserve, we were known to be outside the boundaries of the Reserve. The map and boundary marks are enough evidence which they do have. Secondly, we're implementing our member of parliament's advice that we should not sell our coastal strip because it is very dear to you and your generations to come in the parliament's campaign in 2000.

Thirdly, we do not understand why we should be moved without any proper reasons but among those who view us as too inferior did not bring with them one single animal. We did the job of watching over those animals on our own without Tanapa.

Fourth, we are implementing the promise that our fathers were given by the founder of the reserve Mr. Mahinda that this area is not within the boundaries of the reserve for our benefit and the benefit of our future generations and the nation at large, unless there's contrary information from Mr. Mahinda about the same-such information should be brought forth.

This means that the residents of this sub-village are the ones who requested the government to help preserve our animals as a result of the pain of reckless hunting by people from Pangani, Tanga and Mombasa.

Lastly, we condemn the acts by this government organization that is bringing about a lot of hatred amongst us. We pray that as the District Commissioner, you act on this matter without fear or favour, disregarding societal status, money, etc. Action should be taken against those who caused the death of our brother, and the rumours should be stopped with immediate effect and even those who destroyed the environment by cutting trees and logs meant for the reserve to hastily and greedily build houses and sell them to Tanapa, because such propaganda may reappear in future and what shall it look like this time round! The faith of the residents and the hope they had earlier is slowly dying off because of the leadership of Tanapa.

We are ready to engage anybody in the development of our area which is outside the reserve for our benefit, our generations and the nation without harming the animals or the environment

We wish you all the best!

Hussein Swalehe Akida

Village Chairman

Signature

CC:

Honourable: MP Chalinze

Minister of Tourism and Natural Resources

Minister of Internal Security

Coast Provincial Commissioner

Tanapa Head Office

Editors-Nipashe, Mtanzania and Uhuru Newspapers